NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU
IDARA YA UANDISHI
1 Juni 2018

Kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa

Marafiki Wapendwa wa Kibaha'i,

Kichocheo cha ajabu kilichotolewa na maadhimisho ya miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Baha'u'lláh kwa kazi ya Mpango wa Miaka Mitano kipo dhahiri katika sehemu zote za ulimwengu. Mawazo yanageukia kwenye kumbukumbu ya miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Báb na kile kinachopaswa kutimizwa kabla ya miaka hii mia mbili ya pili, ili kwamba "kila mbegu iliyopandwa kwa upendo kwenye ile ya kwanza" iweze "kulelewa kwa uvumilivu kuelekea utoaji matunda". Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imeomba kwamba tuwasilishe kwenu mambo kadhaa ili kusaidia majadiliano yenu juu ya mada hii. Mnakaribishwa kushirikiana maudhui ya barua hii pamoja na marafiki katika jumuiya zenu kwa jinsi yoyote mnayoona inafaa.

Mfumo mpana kwa ajili ya kuelewa uendeaji wa Ulimwengu wa Kibaha'i kwenye maadhimisho yote mawili ya miaka mia mbili tayari umeainishwa katika barua ya 18 Mei 2018 iliyotumwa kwenu, iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Barua hii ilionesha, mahususi, kwamba sehemu ya shughuli ilitakiwa iwe kwenye ngazi ya mahali. Pia ilielezea zile duru nane zilizopo kati ya kumbukumbu hizi mbili kama kipindi ambapo kiasi kikubwa kabisa cha jitihada iliyohitajika kutimiza malengo ya Mpango wa Miaka Mitano kingehitajika. Huu, kwa hiyo, lazima uwe ndiyo msisitizo mkubwa wa waumini katika klasta zao. Ni msimu wa shughuli za nguvu ambazo zipo mbioni kabisa, na ni chini ya mwaka mmoja na nusu umebakia. Kilichomo katika kipindi hiki chenye thamani kubwa ni Siku Kuu Pacha mwaka huu, kutokana na kuadhimishwa katika muda wa miezi michache tu ijayo. Katika matukio haya, marafiki watapata fursa ya thamani kuchota tajiriba waliyoipata mwaka jana kwa kuwaleta watu pamoja katika maadhimisho ya mahali ambayo huinua mioyo na kuwasha roho.

Maandalizi kwa ajili ya miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Báb hayana budi yafanywe kwa utambuzi kwamba sherehe zinazoashiria kumbukumbu hii zina utaratibu maalumu. Zitatokea miaka miwili tu baada ya miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Baha'u'lláh, na Báb bila shaka alikuwa ni Mtangulizi wa Baha'u'lláh. Kabla na baada ya miaka mia mbili ya kwanza, waumini walizishirikisha familia, marafiki, na watu wa karibu wa aina zote katika mazungumzo kuhusu maisha na mafundisho ya Uzuri Uliobarikiwa, na mazungumzo ambayo yatatokea kuhusiana na sherehe ijayo kwa namna nyingi yatakuwa ni muendelezo wa haya, yakijikita kwa Waasisi wote wawili wa Imani. Kwa kuwa ukuu wa Siku hii, "Siku hii isiyolinganishwa" iliyotukuzwa na Baha'u'lláh, upo dhahiri kutokana na ukweli kwamba ujio wake ulitangazwa na Wadhihirishaji watakatifu wawili, Ambao Siku Zao za Kuzaliwa "zinahesabika kama moja mbele ya Mungu". Katika Yeye Mwenyewe, na katika utokezaji kutoka amri ieneayo ambayo Ufunuo Wake uliileta, umbo takatifu la Báb lilikuwa jibu kwa sala na sihi za vizazi ambavyo vilimngojea Yeye

aliyetabiriwa na Maandiko yote Matakatifu. Kwa ujio Wake, Imani ya Mungu ya milele ilifanywa upya na kuhuishwa kwa wepesi usio wa kawaida. Tena, katika cheo hicho hicho Alichojichagulia Yeye Mwenyewe, Alitukuza kwamba Yeye alikuwa lango kwa Ufunuo bora kabisa ambao, kwa maneno ya Shoghi Effendi, "Alijichukulia Mwenyewe kuwa ni Mtangulizi mnyenyekevu." Jitihada za Wabaha'i kote ulimwenguni za kujitahidi kwa ajili ya utangazaji wa Hoja hukumbusha maonyo ya Báb aliyoyaweka wazi katika Bayan: "Heri ni yake yule ambaye hukazia macho yake juu ya Utaratibu wa Baha'u'lláh, na hutoa shukrani kwa Bwana wake."

Kadiri mipango kwa ajili ya sherehe ijayo ya miaka mia mbili inavyojipatia umbo, bila shaka itaanza kuibuka mifano mingi ya maonesho ya kisanii yakiinukia kutokana na tafakari ya kina juu ya utokeaji kwa mfuatano wa haraka, wa Wadhihirishaji wawili wa Mungu, juu ya upeo wa ulimwengu, na matokeo kwa ajili ya maisha ya binadamu. Mtaona inafaa kujua kwamba Nyumba ya Haki kwa mara nyingine tena inadhamiria kudhamini vyote, filamu na tovuti kwa ajili ya tukio hili. Pia inatazamia kuandaa barua maalum kuashiria sherehe hii ya miaka mia mbili. Tondoti zaidi kuhusiana na haya zitakuwepo wakati utakapowadia.

Sifa ya kutambulika ya sherehe iliyopita ya miaka mia mbili ilikuwa ni idadi ya shukrani kwa Baha'u'lláh na jumbe za pongezi zilizotolewa na waheshimiwa na watu mashuhuri wa jamii, mara nyingi katika kujibu mialiko waliyoipokea kutoa maoni yenye fikra. Walakini, sifa ya tukio hili haichangii yenyewe kwenye majaribio ya kutaka kauli za umma za aina hii. Hata hivyo, juhudi za kuwasaidia watu kama hao zinafahamika zaidi na mafundisho na mambo ya msingi ya Imani, kadhalika jitihada za jumuiya, bila shaka, zingeendelea katika namna ya kawaida.

Katika ujumbe wa Ridván wa mwaka huu, Nyumba ya Haki ilirejea kwenye ushujaa wa Báb na wafuasi Wake, matukio ya kusisimua ambayo maisha yake yana hakika ya kuchunguzwa tena na kusimuliwa tena katika miezi ijayo. Katika kuendana na uendeaji wa jumla kwa sherehe hii ya miaka mia mbili, itakuwa muhimu kutafakari juu ya kusudi la kukumbuka masimulizi haya ya ajabu, ambayo yanastahili sifa kubwa zaidi ya uchunguzi wa historia. Yanawawezesha marafiki, ambao wanajishughulisha na kuitikia mahitaji ya Hoja katika siku hii, kuchota uvuvio na ujasiri kutokana na kujitoa dhabihu kwa wana-mapambazuko. Yaanasaidia kundi la marafiki kutambua kwamba, kwa kujitoa wenyewe kwenye vitendo vya huduma vihitajikavyo katika zama hizi, wanaiga sifa bora za wahenga wao wa kiroho.

Vilele ambavyo kwavyo jumuiya ya Kibaha'i imevifikia hivi karibuni, katika shauku yake kumuenzi ifaavyo "Kiumbe asiye kifani katika muumbo", bado ni dhahiri katika kumbukumbu. Uwezekano utakaoletwa na maadhimisho haya ya pili ya miaka mia mbili, ukifuatiwa kwa ukaribu sana na yale ya kwanza na ukijenga juu ya kile kilichopatikana hapo, hujitokeza kupita kiasi. Muwe na hakika ya sala za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika Makaburi Matakatifu kwa marafiki wote wa Mungu, tukisihi kwamba Baraka za mbinguni ziweze kuwazunguka kwenye kila hatua ya jitihada zao na katika kila kitendo wanachothubutu kwa ajili Yake.

Pamoja na salamu za upendo wa Kibaha’i,

Idara ya Uandishi

Nakala: Kituo cha Mafunzo chA Kimataifa
Bodi za Washauri
Washauri